FEDERAL COURT OF AUSTRALIA

APPEALS

MAHAKAMA YA SHIRIKISHO LA AUSTRALIA

RUFAA

Swahili

Rufaa

Chini ya kifungu cha sheria ya Mahakama ya Shirikisho la Australia ya mwaka 1976 mahakama inaweza kusikiliza rafaa zinazotakana na:

- hukumu ya jaji mmoja iliyotolewa na Mahakama ya Shirikisho bila kujali kama ni amri ya muda au mwisho;
- hukumu ya Mahakama ya Mwisho ya Majimbo ukiachia Eneo la Mji Mkuu wa Australia au Eneo la Kaskazini;
- baadhi ya hukumu za mahakama (ukiacha Mahakama ya Mwisho iliyo na Jopo la Majaji) ya Jimbo, Eneo la Mji Mkuu wa Australia au Eneo la Kaskazini, inavyotekeleza mamlaka ya kisheria kwa mujibu wa Shirikisho;
- baadhi ya hukumu za Mahakama ya Hakimu wa Shirikisho.

Mahakama pia inaweza kusikiliza rufaa kutoka kwa maamuzi ya watu, mamlaka na tume za kisheria ukiachia mahakama. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu namna na mipangilio ya jinsi gani ya kuomba rufaa za aina hii kutoka kwa msajili wa Mahakama yeyote ya Shirikisho na kwenye mtandao wa internet www.fedcourt.gov.au

Nani anasikiliza rufaa?

Rufaa ya hukumu iliyotolewa na Hakimu wa Shirikisho kwenye kesi isiyohusiana na uhamiaji itasikilizwa na Jopo la Majaji wa Mahakama ya Rufaa isipokuwa kama Jaji Mkuu ataona ni sahihi kwa rufaa hiyo kusikilizwa na Jaji mmoja.

Rufaa ya hukumu iliyotolewa na Hakimu wa Shirikisho kwenye kesi inayohusiana na uhamiaji itasikilizwa na Jaji mmoja isipokuwa kama Jaji Mkuu ataona ni sahihi kwa rufani hiyo kusikilizwa na Jopo la Majaji wa Mahakama ya Rufaa.

Rufaa ya hukumu iliyotolewa na Jaji mmoja au Mahakama ya Mwisho mara nyingi inasikilizwa na Jopo la Majaji watatu au zaidi kukaa kwa pamoja.

RUFAA

Unakata vipi rufaa?

Inabidi ujaze iitwayo 'Form 55: Notice of Appeal' tafsiri yake ni Fomu namba 55: Kusudio la kukata Rufaa. Kwenye fomu hii unaitwa mkata rufani 'appellant' kwa kuwa wewe ndio unayekata rufaa.

Fomu halisi ya Kusudio la kukata Rufaa pamoja na nakala kwa ajili ya kila muhusika lazima ziwasilishwe kwenye Mahakama ya Shirikisho. Unaweza kufanya hivi kwa kuziwasilisha kwa kwa Msajili, au kwa kuzituma kwa posta au faksi, au kuzituma kwa kutumia mtandao wa internet.

Hii inaitwa kufungua jalada.

Maelezo zaidi kuhusu kufungua jalada yanapatikana kutoka kwa Msajili na kwenye mtandao wa Mahakama.

Hakikisha unakuwa na nakala ya fomu ya Kusudio la kukata Rufaa kwa ajili yako mwenyewe.

Kama unakata rufaa kuhusiana na uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Jimbo au Eneo, nakala ya fomu ya Kusudio la kukata Rufaa lazima iandikishwe kwenye ofisi ya Msajili, Mhusika au ofisa yeyote wa mahakama hiyo.

Kama maombi yako yamejazwa kwenye fomu sahihi mfanyakazi wa ofisi ya Msajili atagonga muhuri kwenye fomu halisi na nakala/kopi za Kusudio la kukata Rufaa.

Itakubidi uandae utaratibu wa kufikisha nakala zilizogongwa muhuri kwa kila mjibu mashitaka.

Kiwango cha wakati wa kukata rufaa

Hukumu ya muda ni moja wapo, kwa kusema kwa ujumla, inashughulika na mambo yanayohusiana na mpangilio ukiachia uzito wa kesi.

Rufaa itokanayo na hukumu ya muda inaweza kukubaliwa kwa kibali cha Mahakama. Inabidi utume maombi ya kufanya hivyo katika kipindi cha siku 7 kutoka hukumu ilivyotolewa na Jaji wa Mahakama ya Shirikisho au katika siku 21 kutoka siku hukumu ilivyotangazwa na Mahakama nyingine, kwa mfano, Mahakama ya Hakimu wa Shirikisho. Kama muda wa kukata rufaa unakaribia kuisha, unaweza kuomba muda zaidi.

Rufaa ya hukumu ya mwisho inabidi ikatwe katika kipindi cha siku 21 tokea siku hukumu ilipotolewa. Kama muda wa kukata rufaa unakaribia kuisha, unaweza kuomba muda zaidi.

Inagharimu kiasi gani?

Fii inabidi ilipwe wakati unafungua jadala la Kukata Rufaa. Fizi hiyo haita rudishwa kama ukijitoa au kuacha rufani hiyo.

Kama huwezi kulipa fizi hiyo unaweza kuiomba mahakama kuifuta. Watu wengine hawatakiwi kulipa fizi hiyo (kwa mfano, kama umekuwa ukipewa Msaada wa Kisheria 'Legal Aid' au kama mtumiaji wa kadi ya kinga ya afya 'health care card').

Unaweza kupata fomu ya kuomba Mahakama kuondoa au kukupatia msamaha wa kulipa fizi hiyo kwenye ofisi ya Msajili.

Kitu gani kitatokea kama mtu anakata rufaa kupinga uamuzi nilioshinda?

Kama umepewa Kusudio la kukata Rufaa utakuwa unajulikana kama mjibu malalamiko katika rufani hiyo. Inabidi kujaza fomu namba 15 ya Kusudio la Kufika 'Form 15: Notice of Appearance.'

Kama na wewe pia unalengo la kukata rufaa kuhusiana na hukumu ya mwanzo au unataka sehemu ya hukumu halisi kubadilishwa inabidi ujaze fomu iliyobadilishwa iitwayo Fomu 55: 'Notice of Cross-Appeal'.

Kitu gani kitatokea baada ya kujaza jalada la Kusudio la Kukata Rufaa?

Kama tu rufaa hii inatokana na huku iliyotolewa na Hakimu wa Shirikisho, Msajili mara nyingi anweza kuandaa kikao kwa pande mbili ili kuamua ni vitu gani viandikishwe kwenye Mahakama kwenye kitabu cha rufaa.

Sio taarifa zote kutoka kwenye hukumu ya mwanzo zitahitajika. Mpangilio huu unaitwa 'settling the appeal book index'.

Kama rufaa inatokana na hukumu kutoka kwa Hakimu wa Shirikisho isiyohusiana na uhamiaji, Msajili ataweka tarehe ili kusikiliza malalamiko ya pande zote au kusikilizwa kwa rufani hiyo.

Kama rufaa inatokana na hukumu kutoka kwa Hakimu wa Shirikisho inayohusiana na uhamiaji, Msajili atakuandikia barua kuhusiana na muelekeo mzima au amri zilizowekwa na mahakama kuhusiana vitabu vya rufaa, maelezo kimaandishi yanayokubalika na mambo mengine yanayohusiana na usikilizwaji wa rufaa. Msajili atakuandikia tena kukutaarifu tarehe iliyowekwa kwa ajili ya rufaa hiyo kusikilizwa.

Pia utahitajika kufungua jalada mahakamani na kutoa taarifa kwa kifupi kwa mlalamikiwa. Taarifa hiyo lazima iwe na maelezo kwa kifupi ya malalamiko ya kila kipengele kwenye rufaa na weka kesi unazotaka kutumia kutoa hoja zako kusaidia kesi yako. Hii inabidi ifanywe si baada ya siku 5 za kazi kabla ya rufaa kuanza kusikilizwa, ingawa Jaji anaweza kubadilisha kesi.

Usikilizwaji

Utaombwa kuelezea kesi yako kwanza. Mlalamikiwa naye atapewa nafasi ya kujibu. Kisha utapewa nafasi ya mwisho kujibu suala lolote lililoletwa na mlalamikiwa. Unategemewa kuwa na ufahamu wa kilichoandikwa kwenye kitabu cha rufaa na kuwa na uwezo wa kuielekeza mahakama kwenye vifungu vilivyopo kwenye kitabu hicho ili kukusaidia kujenga hoja zako.

Kama utafanikiwa Mahakama inaweza:

- kutoa hukumu tofauti na maamuzi ya awali yaliyotolewa na Mahakama iliyosikiliza kesi mwanzoni.
- kutoa amri ya kesi kusikilizwa tena.

Kuna uwezekano gani wa kufanikiwa?

Kwa rufani yako kufanikiwa inabidi kuishawishi Mahakama kwamba Jaji au Hakimu wa Shirikisho aliyesikiliza kesi mwanzo alifanya makosa na makosa hayo yalikuwa ni muhimu kuweza kuchangia maamuzi kubadilishwa. Baadhi ya mifano ya makosa makubwa ambayo Jaji au Hakimu anaweza kufanya wakati akisikiliza kesi mwanzoni:

Mahakama inayosikiliza rufaa:

- haikubali ushahidi au maelezo yeyote mapya ambayo hayakutolewa kwenye kesi ya mwanzo (labda kwenye mazingira maalum);
- haiwezi kuita mashahidi kutoa ushahidi;
- inasoma taarifa zote za muhimu zilizopo kwenye jalada la kesi mwanzoni;
- inasoma maelezo yote kimaandishi ya sehemu zote za muhimu za kesi ya mwanzo, kama yapo;
- Inasikiliza maelezo yote ya kisheria kutoka pande zote kwenye rufaa.

Ushauri wa kisheria

Kutayarisha Kusudio la kukata Rufaa ni vigumu sana. Kwa hiyo unashauriwa kutafuta msaada wa kisheria ili kuitayarisha kesi yako.

Unaweza kupata taarifa za vyama ambavyo vinaweza msaada wa kisheria bila gharama zozote au kwa gharama nafuu au kutoka kwenye Mahakama au angalia kwenye mtandao wa Mahakama: www.fedcourt.gov.au

Wafanyakazi wa Mahakama hawawezi kutoa ushauri wa kisheria.

Nani analipia gharama za kesi?

Kama ukishindwa kwenye rufaa yako mara nyingi utapewa amri ya kulipia gharama za kesi za mpinzani wako.

Nini kitafanyika kama nikiamua kuondoa rufaa niliyokwishakata?

Unaweza kuondoa rufaa yako kwa kujaza fomu namba 29: Kukusudia kutoendelea 'Form 29: Notice of Discontinuance'. Kama rufaa hiyo haijaanza kusikilizwa hautahitaji kibali cha Mahakama kujaza fomu ya Kukusudia Kutokuendelea. Kama rufaa imeishaanza kusikilizwa, au imeshasikilizwa na Mahakama bado haijatoa hukumu, utahitaji ruhusa ya Mahakama kujaza fomu ya Kukusudia Kutokuendelea.

Kama ukiamua kutokuendelea na rufaa mara nyingi utapewa amri ya kulipia gharama za upande mwingine.

Kukata Rufaa kwenye Mahakama Kuu ya Australia

Hakuna haki ya moja kwa moja ya kukata rufaa kwenye Mahakama Kuu kutokana na uamuzi wa Jopo la Majaji wa Mahakama ya Shirikisho au kutokana na uamuzi wa Jaji aliyesikiliza rufaa kutoka kwenye Mahakama ya Hakimu wa Shirikisho.

Unaweza kuomba kibali toka Mahakama Kuu (kinaitwa 'special leave') ya kukata rufaa, lakini hiki kinatolewa kwenye mazingira maalum tu. Kama ukiomba kibali cha 'special leave' kutoka Mahakama Kuu, nakala ya maombi pia lazima ipelekwe kwa Msajili wa Mahakama ya Shirikisho kwenye Jimbo au Eneo ambapo uamuzi wa mwanzo unaotaka kukata rufaa ulitolewa.

Unaweza kupata wapi fomu?

Unaweza kupata fomu zote zilizoongelewa ndani ya jarida hili kutoka kwa Msajili yeyote wa Mahakama ya Shirikisho. Wanaweza pia kukupatia nakala ya muongozo wa jinsi gani ya kujaza baadhi ya fomu hizo.

Pia unaweza kuzipata hizo fomu na muongozo wa namna ya kuzijaza kutoka kwenye mtandao wa Mahakama: www.fedcourt.gov.au

Wakalimani

Mahakama inaweza kukuandalia mkalimani kuja kusikiliza rufaa. Kama utahitaji mkalimani hakikisha unawasiliana na Msajili wa Mahakama angalau wiki moja kabla ya rufani kusikilizwa.

Kama hutawasiliana na Msajili kuna uwezekano hawataweza kupata mkalimani na usikilizwaji wa rufaa kuhairishwa.

Unaweza kupiga simu 131 450 na kuongea na mkalimani kwenye simu.

MSAJILI WA MAHAKAMA YA SHIRIKISHO

Msajili wa ACT
Commonwealth Law Courts Building
Childers Street
Canberra City ACT 2601
Simu: (02) 6267 0566
Faksi: (02) 6267 0625
TTY: (02) 6267 0537
Email: actman@fedcourt.gov.au

Msajili wa NSW
Level 17, Law Courts Building
Queens Square
Sydney NSW 2000
Simu: (02) 9230 8567
TTY: (02) 9230 8270
Faksi: (02) 9230 8535
Email: nswdr@fedcourt.gov.au

Msajili wa NT Registry
Level 3, Supreme Court Building,
State Square, Darwin NT 0800
Anwani ya posta: PO Box 1806
DARWIN NT 0801
Simu: (08) 8941 2333
Faksi: (08) 8941 4941
TTY: (08) 8982 0838
Faksi ya Kufungulia
Jalada kwa Msajili: (08) 8941 4941
Email: ntreg@fedcourt.gov.au

Msajili wa QLD
Level 6, Commonwealth Law Courts
119 North Quay
Brisbane QLD 4000
Anwani ya posta: P.O. Box 13084
George Street Post Shop
Brisbane QLD 4003
Simu: (07) 3248 1100
Faksi: (07) 3248 1260
TTY: (07) 3248 1272
Email: qldreg@fedcourt.gov.au

Msajili wa VIC
Commonwealth Law Courts
305 William Street
Melbourne VIC 3000
Simu: (03) 8600 3333
Faksi: (03) 8600 3281
TTY: (03) 9670 0320
Email: vicreg@fedcourt.gov.au

Msajili wa SA
Level 5 Commonwealth Law Courts
3 Angas Street Adelaide SA 5000
Anwani ya posta: GPO Box 1350
Adelaide SA 5001
Simu: (08) 8219 1000
Faksi: (08) 8219 1001
TTY: (08) 8219 1011
Email: sareg@fedcourt.gov.au

Msajili wa TAS
Commonwealth Law Courts Building
39-41 Davey Street
Hobart TAS 7000
Anwani ya posta: GPO Box 903
HOBART TAS 7001
Simu: (03) 6232 1715
Faksi: (03) 6232 1701
TTY: (03) 6232 1865
Email: tasreg@fedcourt.gov.au

Msajili wa WA
Commonwealth Law Courts
1 Victoria Avenue
Perth WA 6000
Anwani ya posta: GPO Box A30
PERTH WA 6834
Simu: (08) 9268 7100
Faksi: (08) 9221 3261
TTY: (08) 9325 7053
Email: waregistry@fedcourt.gov.au

Principal Registry
Level 17, Law Courts Building
Queens Square
Sydney NSW 2000
Simu: (02) 9230 8542
Faksi: (02) 9223 7706
Email query@fedcourt.gov.au

02/06